


# Chekechea katika Queensland

## Chekechea ni nini?

Chekechea, inayojulikana kama kindy, ni mpango wa elimu wa muda kwa watoto walio katika mwaka mmoja kabla ya Masomo ya Kabla ya Shule (mwaka wa kwanza wa shule huko Queensland). Chekechea ni mahali ambapo mtoto wako atajifunza kupitia shughuli za kucheza na mwingiliano unaosaidia kujifunza mapema, ustawi na maendeleo. Kwa kushiriki katika chekechea, watoto wanaanza kupenda kujifunza na wanasaidiwa wakati wa kujiunga na Masomo ya Kabla ya Shule.

Mipango ya chekechea iliyoidhinishwa na Serikali ya Queensland hutolewa na mwalimu wa chekechea aliyehitimu. Mipango ya chekechea inaweza kutolewa kwenye vituo vya elimu ya watoto wachanga; shule zilizochaguliwa za vijijini na za mbali na shule zingine zilizochaguliwa za serikali mahali ambapo kumekuwa na vikwazo vya kufikia chekechea; na kwa elimu ya mbali au ya mtandaoni (eKindy) kwa baadhi ya watoto ambao hawawezi kufikia kituoni.

## Kujifunza katika chekechea

Chekechea huwapa watoto wadogo fursa ya:

- kutumia lugha kuwasilisha mawazo, hisia na mahitaji
- kupata marafiki, kuingiliana na kushirikiana na wanafunzi wengine
- kutambua matatizo na kujenga ujuzi wa kuyatatua
- kujiamini na kujitegemea zaidi katika uwezo wao
- kufahamu, kujifunza na kuchangia kwa ulimwengu wao
- kujenga ujuzi wao na kujifunza mawazo mapya, hivyo kuwasaidia kujenga kujiamini kwao.

# Jinsi ya kujiandikisha

Katika jimbo la Queensland, watoto wanaweza kuhudhuria chekechea mwaka mmoja kabla ya kuanza Masomo ya Kabla ya Shule. Kila huduma ni tofauti na baadhi zinaweza kuwa na orodha ya wanaosubiri, kwa hivyo ni vyema kuzungumza na mratibu wa huduma uliyochagua kuhusu wakati mzuri wa kumsajili mtoto wako.

Mtoto wako lazima awe na umri wa miaka 4 ifikapo tarehe 30 Juni katika mwaka anaojiandikisha kushiriki katika chekechea.

| Mtoto aliyezaliwa | Anaweza kuhudhuria chekechea |
|---|---|
| Tarehe 1 Julai 2018 hadi tarehe 30 Juni 2019 | 2023 |
| Tarehe 1 Julai 2019 hadi tarehe 30 Juni 2020 | 2024 |
| Tarehe 1 Julai 2020 hadi tarehe 30 Juni 2021 | 2025 |
| Tarehe 1 Julai 2021 hadi tarehe 30 Juni 2022 | 2026 |
| Tarehe 1 Julai 2022 hadi Tarehe 30 Juni 2023 | 2027 |
| Tarehe 1 Julai 2023 hadi tarehe 30 Juni 2024 | 2028 |

Unachohitaji ili kuandikisha mtoto wako:

- jina na anwani ya mtoto wako
- maelezo yako kama mzazi, mtunzaji au mlezi wake
- maelezo ya amri zozote za mahakama au amri za mahakama kwa mzazi au mipango ya malezi
- maelezo ya usaidizi wowote wa ziada unaohitajika (k.m. ulemavu, mizio ya chakula au mahitaji mengine)
- uthibitisho wa tarehe ya kuzaliwa (k.m. cheti cha kuzaliwa)
- hali ya kiafya na ya chanjo
- maelezo ya watu wanaoruhusiwa kumchukua mtoto wako na mtu wa kuwasiliana naye wakati kuna dharura.

Mtoa huduma wako ataweka maelezo haya kwa usiri na utakuwa na ufikiaji kamili wa rekodi za mtoto wako.

# Jinsi ya kuchagua mpango wa chekechea

Watoto wote katika jimbo la Queensland wanastahiki kuhudhuria mpango wa shule ya chekechea ulioidhinishwa mwaka mmoja kabla ya kujiunga na Masomo ya Kabla ya Shule.

Mpango ulioidhinishwa wa chekechea hukidhi mwongozo wa serikali, na ni:

- mpango wa kujifunza unaotolewa na walimu wa chekechea waliohitimu, kwa mujibu wa mwongozo wa serikali
- kwa kawaida hutolewa kwa saa 15 kwa wiki, wiki 40 kwa mwaka, kwa watoto katika mwaka wa Masomo ya Kabla ya Shule
- unaofuata mwongozo wa kujifunza wa chekechea ya jimbo la Queensland au mpango mwingine wa elimu ulioidhinishwa na Mamlaka ya Mitaala na Tathmini ya Queensland.

Ili kupata usaidizi wa kutambua mpango ulioidhinishwa na Serikali ya jimbo la Queensland, tafuta 'alama ya tiki ya kindy inayoonyesha kuwa umeidhinishwa', hiyo ndiyo picha iliyo hapa chini.

Kindergarten Approved Program Queensland Government

# Gharama za chekechea

Kuanzia 2023, Serikali ya Queensland inafanya chekechea kuwa bei nafuu kwa familia nyingi za Queensland. Iwe unahudhuria chekechea katika chekechea za kipindi kifupi au chekechea katika kituo cha utunzaji wa kutwa unaweza kustahiki kupata chekechea bila malipo au kwa bei nafuu.

Ada za chekechea hutofautiana kulingana na huduma. Wasiliana na mratibu wa huduma ya chekechea unayopendelea kwa maelezo kuhusu ada zao. Unaweza pia kutembelea **www.qld.gov.au/Kindysavings** ili kuangalia ikiwa unastahiki huduma za chekechea za bei nafuu au za bila malipo.

Huduma za chekechea za bila malipo au za bei nafuu hutolewa kwa familia zinazostahiki, ikiwa ni pamoja na familia zinazolea au kuwatunza watoto wasio wao, ambazo:

- wana Kadi ya Huduma ya Afya ya Serikali ya Australia (HCC) (au zina mtoto aliye na kadi hiyo)
- wana Kadi ya Watu Waliostaafu ya Serikali ya Australia (haki ya moja moja ya kupata huduma za HCC)
- wana Kadi ya Dhahabu au Kadi Nyeupe ya Idara ya Masuala ya Watu Waliokuwa Wanajeshi
- wana mawasiliano rasmi, kama vile barua, kutoka kwa wakala husika inayoeleza nia ya kuwapa HCC
- zina ushahidi wa mipango rasmi ya utunzaji wa watoto wasio wao au malezi ya jamaa zao
- wanatambulika kama Wazawa wa Australia na/au Wenye Asili ya Visiwa vya Torres Strait (au zina mtoto aliye na utambulisho huu)
- wana watoto watatu au zaidi, wenye umri sawa, walioandikishwa katika mwaka mmoja
- wana mtoto ambaye ametambuliwa kuwa anaishi katika mpangilio rasmi wa ulinzi wa mtoto nje ya mpangilio wa utunzaji wa nyumbani
- wameingia Australia chini ya Mpango wa Wakimbizi na Kibinadamu wa Serikali ya Australia, au wako katika harakati za kutafuta hifadhi na zina visa ya muda.

Fedha za ruzuku kwa ajili ya chekechea ya bila malipo au ya bei nafuu hutolewa moja kwa moja kwa mtoa huduma wako. Inaweza kupunguza gharama unazolipia kutoka mfukoni mwako. Unaweza kupewa mara moja pekee, hata kama umetimiza vigezo vingi.

Familia zinazostahiki kupata Pesa za Serikali ya Australia za Kusaidia Familia Kulea Watoto pia zinaweza kustahiki ada zilizopunguzwa.

Familia za watoto zinazoshiriki katika mpango wa kindy katika mpangilio wa utunzaji wa mchana kutwa zinaweza pia kustahiki Ruzuku ya Utunzaji wa Watoto ya Serikali ya Australia.

Maelezo kuhusu kustahiki ruzuku hizi za Serikali ya Australia inapatikana katika Centrelink.

Kwa maelezo zaidi
Tembelea **www.qld.gov.au/kindy**

220233